Sheria Kamilifu Ya Uhuru (The Perfect Law of Liberty)

Na

J. D. Logan

Sheria Kamilifu Ya Uhuru

Na

J. D. Logan

Novemba 6, 2011

Sheria Kamilifu Ya Uhuru

"...aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwakwe." (Yak. 1:25).

Katika mistari hii tunapata wajibu wa Wakristo wote, pasipo hayo hakuna atakaye barikiwa. Baraka ya Mungu husemwa katika kujaribu kutangaza "sheria kamilifu" katika njia nne.

- "kuitazama kwa makini"
- "endelea kuifanya"
- Tusisahau tunachosikia"
- Lakini kufanya hili"

Kwa sasa Yakobo anagusia umuhim wa "sheria" hii. Kwanza anaiita "kamilifu". Pili tukiisoma na kuiacha (kutofanya inachosema), hatuoni mbali, hatuwezi kukumbuka kilicho mhimu, na kuwa kama mtu ambaye hawezi kujitambua baada ya kujitazama kwenye kioo.

Kwa shauri la umuhimu iliyowekwa katika "sheria" hii, ni muhimu kwamba tukaangalia kilichoanzisha sheria katika maandiko. Tunaangali nini tunapo tafuta mamlaka na asilimia katika maandiko?

Usi? Usifanye Hivi?

Kama mtu anatafuta maagizo ya aina hii katika Agano Jipya, inakuwa wazi haraka kwamba kuna uchache wake. Je hii inamanisha kwamba tuna maagizo machache katika Agano Jipya? Sio kweli!

Kuna njia nyingi zimetumiwa na Roho Mtakatifu kuonyesha mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu zaidi ya ukali "usi" au "usifanye."

Napenda kulinganisha hili na jinsi tunavyowaongoza wanyaama kwenye nira. Mtu ni lazima awe mkali kwa ng'ombe

maana hawana akili. Tunawachapa kwa fimbo, tunatumia mijeledi, n.k. hii ni sawa na agizo la moja kwa moja. Je tunahitaji hili? Ndiyo wakati fulani tunahitaji!

Kwa upande mwingine, hivi sivyo ambavyo Baba yetu anavyotuongoza wakati mwingi. Kinachofuaata ni kuangalia njia nyingi tunavyoongozwa na neno la Mungu.

"Agizo"

Tunapo "agizwa" na Yesu au mitume wake ili kufanya kazi fulani, tunawajibishwa kutii kuliko tunavyosoma "usi", n.k.

Paulo anaeleza, "*Uwakumbushe mambo hayo ukiwaonya machoni pa Mungu, wasiwe na mashindano ya maneno, ambayo hayana faida, bali huwaaribu wasikiao.*" (2 Tim. 2:14).

Kuhusu neno "agiza", kamusi ya Strong inatafsiri kama "diamarturoma" [1263] "kujaribu au shindana kikamilifu au [kwa mat] kikamilifu (kuhubiri-JDL):-agiza, shuhudia (kwa), shahidi."

Paulo anamuagiza Timotheo, "*Nakuagiza mbele za Mungu na mbele za Kristo Yesu, na mbele zaa malaika wateule, uyatende hayo pasipo kuhukumu kwa haraka; usifanye neno lolote kwa upendeleo.*" (1 Tim. 5:21).

Ni vyema kutambua kwamba Paulo hakutumia neno la faragha "usifanye", n.k katika waraka wake wote kwa Timotheo, bado anamuagiza kuitunza pasipo upendeleo.

Paulo aalimuagiza Timotheo. "*Mwanangu Timotheo nakukabidhi agizo hilo liwe akiba, kwa ajili ya maneno ya unabii yaliyotangulia juu yako, ili katika hayo uvipige vile vita vizuri.*" (1 Tim. 1:18).

Maneno yaliyotumiwa katika kifungu hiki ni "paraggello" [3853] "kuambukiza ujumbe", n.k [kwa matu] kuunganisha;-[kujiingiza] agizo, [toa] agiza, tangaza."

Matumizzi tofauti ya neno "agizo" yanafuata kwa ufupi:

- 1 Tim. 1:3, "*...UWAAGIZE wengine wasifundishe elimu nyingine...*"
- 1 Tim. 5:7, "*...mambo hayo pia uwaagize ili wasiwe...*"
- 1 Tim. 6:13, "*Nakuagiza mbele za Mungu...kwamba uilinde...*"

Lakini zaidi yah ii, neno linalofanana na hilo hutolewa kama “agizo” katika yafuatayo, na nitaziorodhesha kwa uchaache. Msomaji anashauriwa kuzisoma kwa ukamilifu wao ili kuangalia ulinganifu wao.

- Mdo. 16:18
- 1 Kor. 7:10
- 2 Thes. 3:4-6
- 1 Tim. 4:6
- Mdo. 10:42
- 1 Thes. 4:11
- 2 Thes. 3:10

Ni lazima tutambue maagizo yote yaliyotolewa na Yesu na mitume kama maagizo na kuyaweka katika hiyo “sheria kamilifu.”

“Ushuhuda”

Mengi huelekeza katika “ushuhuda” wa Yesu na mitume hupatikana katika Agano Jipya. Neno linalotokana na neno “maturion”, Strong [3142] na hutoholewa kama “kitu chenye ushahidi, i.e (jum) ukweli uliotolewa au (dhan) uamzi (katika hema takatifu): kushuhudiwa, ushahidi, shahidi.”

Paulo aliliambia kanisa la Korintho, “*Kwa kuwa katika kila jambo mlitajirika katika yeye, katika maneno yote, na maarifa yote; kama ushuhuda wa Kristo ulivyothibitika kwenu.*” (1 Kor. 1:5-6).

Zaidi, tunapata Paulo akiongea katika 1 Kor. 2:1, “*Basi ndugu zangu mimi nilipokuja kwenu, sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno wala kwa hekima.*”

Na katika 2 Thes. 1:10, Pulo anasema, “*…ushahidi wetu (wa mitume) miongoni mwenu uliaminiwaa…*”

Pia katika 2 Tim. 1:8, “*Basi usiuonee haya ushuhuda wa Bwana wetu, wala usinionee haya mimi mfungwa wake, baali uvumilie mabaya pamoja nami kwa ajili ya Injili, kwa kadiri ya nguvu ya Mungu.*”

Kwa maneno haya, tunashawishiwa kwamba “shuhuda zote” za Kristo na Mitume pia ni sehemu ya hiyo “sheria kamilifu.”

“Mapokeo”

Wengine wanaweza kupinga matumizi ya desturi katika mafunzo ya “sheria kamilifu”. Hataivyo, hatupaswi kuondoa somo hili nje ya mikono yetu kwa sababu kuna mifano endelevu ya kuweka desturi fulani katika hii “sheria kamilifu.”

Paulo anatundisha katika 2 Thes. 3:6, “*…jitengeni nafsi zenu na kila ndugu aendaye bila utaratibu, wala si kwa kufuata mapokeo mliopokea kwetu.*”

Pia katika 2 Thes. 2:15, “*Basi ndugu simameni imara mkayashike mapokeo mliofundishwa, ama kwa maneno, ama kwa warakaa wetu.*”

Neno mapokeo katika kifungu hiki ni “paradosis” Strong [5862], “kuhaamisha, dhana, : hadhira, desturi.”

Kwa maelezo ya utohoaji “maagizo” hapo juu, tafadhali angalia 1 Kor.11:2, “*Basi nawasifu kwa sababu mmenikumbuka katika mambo yote nanyi mmeyashika yale mapokeo vile vile kama nilivyowatolea.*”

Katika kifungu hiki tunaona kwamba “mapokeo” ya mitume yalikuwa, hasa maagizo na laazima kwa umuhimu yajumuishwe katika hii “sheria kamilifu.”

“Kielelezo”

Mtu hawezi kujifunza “sheria kamilifu” bila kujuaa matumizi ya mifano iliyofunuliwa kwetu katika maandiko. Kuna mifano ya Yesu, mitume, na watakatifu waanaume kwa wanawake wa zamani. Pia kuna mifano ya kanisa la kwanza ambayo haipaswi kuachwa. Zipo matendo ya dhambiyanayshikiliwa kama mifano mizuri ambazo hatupaswi kufuataa. Kuangalia machache:

- Yoh. 13:15, “*Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, naanyi mtende vivyo.*”
- Yak. 5:10, “*Watwaeni…manabii…wawe mfano…*”
- Heb. 4:11, “*…ili kwamba mtu yeyote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi.*”

Nimetoa haya kwa ufupi kwa kukosa nafassi. Ningependa kuwasihi nyote msome vifungu hivi kwa ukamilifu wake.

“Vielelezo” huchukuliwa kutoka katika neno “hupodeigma” ikimanisha onyesha kwa kufuata au onya (hal. maalum, kinga) en-(mf) ano, kielelezo.”

Petro anaaonyesha mfano: Yesu. *“…maana Krsito naye aliteswa kwa ajili yenu akawaachia kielelezo, mfuate nyayo zake.”* (1 Pet. 2:21)

Neno lingine linalotumiwa kwa “mfano” ni “Tupois” [5179] Strong. Hutoholewa kama , miongoni mwa maana nyingine, “kufa, kama kupigwa, umbo, aina, ie, (kiel) mtindo (wa kufuatwa) au (kwa kuonya): en (mf)ano, mtindo, umbo, aina, mfanano, kielelezo…”

Zifuatazo ni mifano ya matumizi haya.

Vielelezo

- 1 Tim.4:12, “*…uwe mfano kwao waaminio…*”
- 1 Kor. 10:6, “*…mambo haya yalikuwa mfano kwetu…*”

Mfano

- Fil. 3:17, “*…kama tulivyokuwa mfano kwenu…*”
- 2 Thes. 3:9, “*…sisi wenyewe tumekuwa vielelezo kwenu…*”

Mtindo

- Mdo. 7:44, “*…sawasawa na mfano ule aliouona…*”

Umbo

- Rom. 5:14, “*…aliye mafano wake yeye atakayekuja…*”

Namna

- Rom. 6:17, “*…ile namna ya elimu…*”

Kielelezo

- Tito. 2:7, “*…kielelezo cha kazi njema…*”
- Heb. 8:5, “*…kulingana na kielelezo aliokuonyesha…*”
- 1 Tim. 1:16, “*…mfano kwao wasio…*”

Kutoka katika fungu hivi tunaweza kuona umuhimu wa vielelezo inayopatikana katika Agano Jipyaa. Kuna mifano ya kanisa la kwanza, pasipo hilo tusingekuwa na ujuzi wa kuabudu kama kusanyiko. Kuna mifano ya mienendo binafsi, mabaya na mazuri kwa ajili ya kujifunza kwako, tunapoonywa ili kuwa mifano ya waaminio.

Kutokana na haya, mtu anawezaje kuwa naa mashaka kuhusu ujumuisho wa mifano ya kimaandiko katika "sheria kamilifu?"

"Mashaidi"

Katika mitazamo ya ujuzi wa mwanadamu, ukweli mmoja unaabaki. Ili neno liwe kweli mtu ni lazima awe na mashaidi au shahidi katika jambo lenyewe.

Chini ya sheria ya Musa, ukweli ulionekana chini yaa mashaidi wawili au zaidi (Heb.10:28).

Paulo anatufundisha kwamba tusipokee mashitaka yaliyo chini ya shaidi wawili (1 Tim. 5:19)

Hataivyo, hakuna sababu ya kuwa na mashaidi wengi ili ukweli uweze kudhihirika kutokana na mssimamo wa Agano Jipya. Yesu alifundisha, "*…mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.*" (Mat. 4:4).

Inaonekana kwamba Yesu alizingatia kwamba neno likisemwa mara moja linatosha: hakuna sababu ya kuchunguza zaidi (hataivyo kuboresha inaongeza nguvu katika ukweli).

Yesu alimwambia Nikodemo, "*…twanena kilie tulijualo, na kushuhudia tulichokiona, wala hamkuukubali ushuhuda wetu.*" (Yoh. 3:11).

Vifungu vingi katika Agano Jipya humshuhudiaa Yesu kwa injili ya ufalme. (angalia Yohana 5).

Yesu aliwaambia mitume wake, "*Nanyi mtakuwa mashaidi wangu, maana mmekuwa pamoja nami tangu zamani.*" (Yoh. 15:27). Mitume ni mashahidi wanaokubalika kwa ajili ya kweli.

Katika uongofu wake, Anania alimwambia Paulo, "*Na wewe utakuwa shahidi wake (Yesu) kwa watu wote kwa yale uliyoona na kusikia.*" (Mdo. 22:15). Paulo anaboresha hili katika Mdo. 26:16, "*…nikuweke wewe uwe mtumishi na shahidi wa mambo haya*

uliyoyaona, na wa mambo ambayo katika hayo nitajidhihirisha kwako."

Ni wazi kwamba Yesu aliendelea kumuongoza Paulo kutia mambo mengi na ni wazi zaidi kwamba Paulo aaliendelea kustawi na kuongozwa katika yote aliyofundisha na kutenda.

Tunapoangaalia mafundisho na matendo ya mitume katika kanisa la kwanza, tunajua kwamba ni kwa ajili ya kutuongoza. Mashahidi hawa ni sehemu muhimu ya "sheriaa kamilifu."

"Maneno Ya Mitume"

Paulo anafundisha. "*Mambo mliojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia, na kuyaona kwangu, yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi.*" (Fil. 4:9).

Yote haya yanajumuishwa. Kufupishaa haya, zingatia:

- Mambo walijifunza kwa Paulo.
- Mambo yaliyopokea (kutoka kwa Paulo kupitia wengine)
- Kusikia kwa Paulo (mazungumzo)
- Kuona kwangu. (mwenendo wa maisha yake katika kanisa.)

Katika njia hizi nne Paulo alifundisha yote yaliyomzunguka, na katika haya manne ameagiza "FANYA".

Soma katika Matendo ya mitume kuhusu maisha ya Paulo baada ya kuongolewa alipokuwa akitembea miongoni mwa wakuu wake, Wayahudi. Mfuatilie alipokuwa akiwatembelea mapagani, akifundisha injili. Muone kama mtenda kazi, akianzisha makussanyiko kadiri alivyokuwa anakwenda, na kurudi ili kujua yalivyokuwa yanaendelea. Katika mambo haya yote aameaagiza, "FANYA"

Haishangazi kwamba kwa ukweli huu kwamba Paulo angeweza kuandika. "*Ndugu zangu mnifuate mimi mkawatazame wao waendao kwa kuufuata mfano tuliowapa ninyi.*" (Fil. 3:17).

Pia 2 Thes. 3:9, "*...ili tuwe mfano kwenu mtufuate...*"

Katika 1 Kor. 14:37, "*Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana.*"

Na 2 Pet. 1:3, "*Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa…*"

Tunawiwa kuweka maneno yote ya mitume katika "sheria kamilifu".

Haya, basi, ni vifaa vya hiyo "sheria kamilifu".

- Agizo la moja kwa moja la Kristo na mitume wake
- Agizo lililotolewa na watu ao hao
- Ushuhuda wa Yesu na mitume
- Mapokeo ya mitume
- Mifano ya mitume na kanisa la kwanza
- Ushahidi wa watu waliovuviwa
- Maneno na matendo ya mitume

Katika kuupenda kweli,

J D Logan